UJIFUNZAJI WA BIBLIA WA WITO WA LAMBETH
UHUSIANO BAINA YA IMANI

UTANGULIZI

Nyenzo hizi za Kujifunza Biblia zimeandaliwa kama sehemu ya Awamu ya 3 ya Lambeth Conference na Miito ya Lambeth. Ujifunzaji huu wa Biblia unahusu Wito wa Lambeth kuhusu Uhusiano baina ya Imani. Unaweza kusoma Wito wa Lambeth hapa.

Jinsi ya kutumia somo hili

'Wito na Mwitikio' – Muundo wa Kujifunza Biblia

Kila moja ya Miito ya Lambeth hutolewa kwa Ushirika wa Anglikana – ikihitaji mwitikio. Ujifunzaji wa Biblia upo katika muundo wa 'Wito na Mwitikio'. Ujifunzaji huu wa Biblia kuhusu Uhusiano baina ya Imani utakupitisha katika hatua tatu:

1. Sikia Wito

Soma Wito wa Lambeth na hasa Uthibitisho wake (Sehemu ya 3) kuhusu mabadiliko ya muktadha ambamo tunaishi na changamoto zinazoongezeka kwa jamii za Kikristo katika nchi ambazo wakristo ni wachache. Pia soma na usikie Maombi Maalum (Sehemu ya 4).

2. Sikiliza Maandiko

Rejea kwenye Maandiko ili kutia nanga na kuimarisha tafakari hii, hasa katika Yohana 4 mistari 1 hadi 30, maelezo yanayomwonyesha Yesu akizungumza na mtu wa imani nyingine, mwanamke Msamaria, na akishuhudia injili. Tunaweza kujifunza nini kutokana na kifungu hiki kuhusu jinsi tunavyohusiana na watu wa imani nyingine?

3. Onyesha Mwitikio

Jadili jinsi wewe na jumuiya ya kanisa lako mnavyoweza kuwasiliana na watu wa imani nyingine katika muktadha wa mahali ulipo kulingana na kile ulichojifunza kutoka kwenye maandiko.

Anza

1. Sikia Wito (dakika 15)

Soma Wito wa Lambeth kuhusu Uhusiano baina ya Imani. Unaweza kusoma Wito wa Lambeth hapa.

Tafakari hasa kuhusu Uthibitisho wake (Sehemu ya 3) kuhusu mabadiliko ya muktadha ambamo tunaishi na changamoto zinazoongezeka kwa jamii za Kikristo katika nchi ambazo wakristo ni wachache. Pia soma Maombi Maalum (Sehemu ya 4) hasa ya kwanza (4.1), wito wa kushuhudia majirani zetu wa desturi zingine za kidini, kwa maneno na matendo, na kupitia huduma ya unyenyekevu.

- Hii yote inazungumzaje na wewe?
- Je, tayari unashuhudiaje watu wa imani nyingine kupitia maneno yako, matendo na kupitia kuwatumikia?
- Ikiwa unaishi katika eneo ambapo Wakristo ni wachache, ni vizuizi na mashinikizo gani unayokabiliwa nayo, pia ni fursa gani zilizopo?

2. Sikiliza Maandiko (dakika 25)

Rejea kwenye Maandiko ili kuleta msukumo na kuongoza tafakari hii. Anza kwa kusoma Yohana 4 mstari wa 1 hadi 30, ambayo inaonyesha Yesu akizungumza na mtu wa imani nyingine, mwanamke Msamaria, na akishuhudia injili. Tunaweza kujifunza nini kutokana na kifungu hiki kuhusu jinsi tunavyohusiana na watu wa imani nyingine?

Ni muhimu kutambua kwamba ingawa Wayahudi na Wasamaria walikuwa na asili moja katika imani ya Abrahamu, Isaka na Yakobo, na Musa na Kutoka, tangu Dola ya Ashuru ilipovamia na kuharibu ufalme wa kaskazini wa Israeli na mji mkuu wake Samaria mnamo mwaka 722 KK (kabla ya Kristo), watu wa nchi hiyo na Wayahudi wa Galilaya na Yuda walikuwa wameendelea kuwa na imani na tamaduni zilizokuwa zinaendelea kuwa na tofauti kubwa. Aidha, wakati wa Yesu walikuwa ni maadui (angalia, kwa mfano, Luka 9.51-6, ambapo kijiji cha Wasamaria kinakataa kumkaribisha Yesu na wanafunzi).

Gundua kwamba

- mazungumzo na urafiki kati ya Yesu na mwanamke Msamaria ulianza kwa sababu Yesu alikuwa amechoka na ana kiu. Atakuwa alikuwa ametambua udhaifu wake na hitaji la kibinadamu na kwa hivyo akawa tayari kuwa na mazungumzo naye.

- Mwanamke huyo alienda kuteka maji majira ya adhuhuri, jambo linalomaanisha wakati ambapo jua ni kali zaidi wakati ambapo hakukuwa na wanawake wengine. Hii inaonyesha alikuwa mtu aliyetengwa na jamii inayoheshimika na kwa hivyo pia alikuwa katika mazingira magumu.
- Kiutamaduni, akiwa mwanaume wa Kiyahudi, Yesu hakupaswa kuzungumza na mwanamke Msamaria, lakini alikuwa tayari kuvunja mwiko huu wa kitamaduni. Angeweza kufanya hivi kwa sababu alikuwa katika mazingira magumu na kwa hivyo hakutaka kumlazimisha mwanamke, ingawa bado anahoji haki yake ya kufanya hivyo (mstari wa 9).
- Kutokana na mazingira haya magumu Yesu anaweza kushuhudia kile anachotaka kumshirikisha, ambacho ni maji yaliyo hai (mstari wa 10).
- Mwanamke anaonyesha kuwa na werevu hapa na udadisi kwa kumhoji Yesu jinsi atakavyompa maji wakati, kwa kuwa ni Myahudi, hana haki ya kuchota maji kwenye kisima hiki.
- Kisha Yesu anaanza kuzungumzia maji ya kimwili na anazungumzia maji ya uzima ya kiroho ambayo anaweza kutoa na mwanamke huyo anaitikia kwa shauku ukarimu huu, ingawa bado anafikiria kuhusu maji ya kimwili. Hii inaonyesha uhusiano wa kuaminiana unaongezeka kati yao.
- Baadaye Yesu anahamishia mazungumzo kwenye hali ya maisha yake mwenyewe na ndoa zake nyingi. Kwa uelewa wa kina wa kiteolojia mwanamke kisha anapeleka mazungumzo kwenye kiwango kingine kwa maoni yake, ambayo kwa kweli ni swali, kuhusu imani yao, ya Wasamaria na Wayahudi, ipi ni ya kweli.
- Hii inamruhusu Yesu kushuhudia ukweli ambao amekuja kumshuhudia yeye na wengine, kuhusu imani mpya ambayo inapita ile ya Wasamaria na Wayahudi.
- Hii inamfanya mwanamke kushuhudia imani yake mwenyewe kuhusu Masihi ajaye na atakayetufunulia ‘mambo yote‘(mstari wa 25). Hili linafanya Yesu ajibu kwa kujishudia mwenyewe, kwamba *yeye ndiye* Masihi huyo (mstari wa 26);
- Kutokana na uhusiano huu wa kila mtu kugusa hisia za mwenzake, kuaminiana na kila mtu kumweleza mwenzake hisia zake kunatokana na safari ya uinjilisti ya ajabu ya mwanamke huyo kurudi mjini kwake na kwa watu wake kuwaambia kuhusu nabii huyu na uwezekano kwamba anaweza kuwa Masihi!

Tunaweza kujifunza nini kutokana na kifungu hiki kuhusu jinsi tunavyoweza kuhusiana na watu wa imani nyingine?

3. Onyesha Mwitikio (dakika 20)

Ni kwa jinsi gani aya kutoka katika injili ya Yohana inakusaidia na kukuhimiza kuingia katika uhusiano na watu wa imani nyingine na kuuendeleza?

Wewe na jumuiya ya kanisa lako mnawezaje kuitikia Wito wa Lambeth, hasa Ombi Maalum la kwanza (4.1), kushuhudia majirani zetu wa desturi zingine za kidini, kwa maneno na matendo, na kupitia huduma ya unyenyekevu?

Unawezaje kusaidia jambo hili litokee? Nini kinachohitajika?

Unawezaje kuitikia ombi maalumu la tatu, ‘Kwa viongozi wa jumuiya nyingine za imani, kujiunga pamoja nasi katika kuchunguza jinsi tunavyoweza kuwezesha kazi ya ushirikiano zaidi katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na changamoto nyingine katika mazingira yetu ya pamoja, kupunguza umaskini na kuwajali walio katika mazingira magumu’ (4.3)?

Unawezaje kuitikia Ombi Maalum la sita, ‘Kwa sisi sote ambao ni wanafunzi wa Kristo, kujitolea kuliombea Kanisa linaloteswa katika juhudi zake za kuendelea kuhusika kwa upole na kushuhudia imani hata katikati ya uadui na mapambano ili kujenga uhusiano imara na majirani wa imani zingine.’

Ni hatua gani rahisi ambazo wewe na jumuiya ya kanisa lako mnaweza kuchukua ili kupeleka mbele mambo haya?

Ombi la Kuhitimisha

Mungu wa watu wote, fungua mioyo yetu kuelewa desturi nyingine za imani. Sisi sote tumeumbwa kwa mfano wako na tunatafuta kujua na kufuata njia zako, kukusifu, na kuwa vyombo vya uwepo wako Mtakatifu. Tusaidie tuwaheshimu wale ambao wako tofauti na sisi, ambao wanafuata desturi tofauti wa imani. Tusaidie tutafute kujua ukweli wa Neno lako na kupata msingi wa pamoja katikati ya desturi nyingi za imani na tutambue kwamba sisi zote ni binadamu. Tusaidie kuwa watu wa huruma na uelewa, tukiunda njia ya kuishi kwa amani pamoja na watu wote. Amina.

(Imetolewa kwa shukrani kwa Masista Wadominika wa Amani).